# Ufunuo wa kifuniko

*1Petro2:1-10; "Mmwendee yee, jiwe lililohai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yalio hai, mmejengwa kwenye nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya yesu kristo. Kwakuwa imeandikwa katika maandiko, Tazama, naweka katika sayuni jiwe kuu la pembeni,teule lenye heshima, Na kila amwaminie hatatahayarika. Basi hecshi hii ni kwenu ninyi mnao amini………..*

sikiliza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu Bwana ndie mmoja (kumbukumbu 6:4). Hilo hapo tena. Yehova wa Agano la kale ni yesu kristo wa Agano Jipya, Agano jipya halifunui Mungu mwingine bali ni muendelezo wa ufunuo ule wa Mungu yule yule alie mmoja. Kristo hakuja huku chini kujifunua yeye Mwenyewe alijulikana hakuja kumfunua Mwana. Alikuja kumfunua na kumfanya Baba ajulikane. Kamwe hakuzungumza juu ya Miungu miwili; Amezungumza juu ya Mungu MMOJA. Na sasa katika wakati huu wa mwisho, tumerudi tena katika ufunuo wa kifuniko, ufunuo ulio wa muhumu sana katika Biblia yote ufunuo wa uungu, ambao ni yesu ni Mungu, Yeye na Baba ni mmoja: Kuna Mungu mmoja, na Jina lake ni BWANA YESU KRISTO. (matendo 2:36; 1yohana 5:43) [1]

Hizi tabia (2petro 1:3-11) lazima ziwe pale kabla ya kile kifuniko kuja juu yake. Oh.unaweza kupiga kelele, unaweza ukaimba, unaweza ukanena kwa lugha na kucheza—hilo halina uhusiano na hilo hata kidogo, mpaka haya mambo kimaandiko yamethibitishwa kuwa yamewekwa mhuri ndani yako…….. roho mtakatifu amekutia muhuri kama mtu binafsi. Hapa sasa u mwana na Binti [2]

Kwanza; kimsingi, ni lmani. Pili: ongeza katika lmani yako, nguvu; katika nguvu, maarifa, kutoka maarifa, kiasi; kutoka kiasi subira; katika subira, kuwa kama Mungu; kutoka kuwa kama Mungu Upendano wa kindugu, kutoka upendano wa kindugu; halafu kile kifuniko ambacho ni Upendo: vitu saba.



Na sasa kama ilivyokuwa mtu binafsi, hizi tabia na mambo haya ni (maarifa na kiasi)—vinaongezwa kwenye lmani yetu, halafu kile kifuniko kinapokuja, Roho mtakatifu anavifungamananisha vyote pamoja; hapo unapata ubatizo wa Roho mtakatifu. Hiyo ndio sababu umepunguka leo.

Sasa, mshiriki anapozaliwa na roho mtakatifu katika familia ya Mungu na amethibitishwa anazo hizi tabio ndani yake. Kwamba Mungu angeweza kuona tabia, maarifa, kiasi, subira, upendano wa ndugu, na utauwa (kuwa kama Mungu) ndani yake, hapo sasa Mungu anamtia yeye mhuri au anamuadhimisha mwana. Na hapo, sasa ndipo utaona wana na binti za Mungu. [3]

Ninamsihi yeye kwa moyo wangu wote kwamba kwa msaada wake na kwa neema, ninaomba kwamba nitatafuta kila siku bila kukoma mpaka nijisikie kwamba hayo yanayohitajika yanatiririka katika umbile langu hili; Mpaka niwe udhihirisho wa kristo alie hai/aishie; kwa maana alifanyika dhambi kama mimi, ili kwamba niweze kuwa haki ya Mungu kama yey (1korntho 1:30). Alichukuwa mahali pangu Bwana niwezeshe nichukuwe mahali pake sasa maana hilo ndilo kusudi lake la kutufia.

Sasa katika kujenga huu mjengo, kijenga hiki kimo inaanza na msingi ambao ni Imani, Nguvu, Maarifa, Kiasi, Subira, kuwa kama Mungu (utauwa), Upendano wa kindungu. Sasa, Itafanyaje? Hapo wanasubiri kile kifuniko ambacho ni upendo; [4]

Na mtu yeyote anajua Mungu ni upendo [3]

Mungu ni upendo (1yohana 4:16) na Anatawala, na yeye ni nguvu ya kila kimoja ya vita hivi (tabia). Ndio Bwana Hiyo nisawa hapa, Hiyo nisawa hapa. Unaona. Nimeingia katikati ya kazi hizi zote hapa, na hapa kuna mawimbi kidogo yanayokuja. Hiyo ni nini? Roho mtakatifu akija chini kutoka kwa kristo, Roho mtakatifu, Roho mtakatifu yuko juu ya hivi vyote akivifunga\kuvishikilia vyote pamoja akijenga nini? Kanisa kamilifu kwa ajili ya kile kifuniko kilijie. Kumekuwa kunafanyika nini tena? Imedhihirishwa katika nyakati saba za kanisa na wajumbe saba wa kanisa [4]

Hebu niseme na mimi kitu Fulani wakati wa kuungana- unaona makanisa yanayoungana, mataifa yanaungana--- Ni wakati wa Mungu kuungana na Bibi Arusi wake pia. Na ninasema hili kwa kicho na

heshima. Ninaamini Bibi Arusi wa kristo ameitwa; naamini Ametiwa mhuri katika ufalime wa Mungu. Ninaamini mitambo yote ipo pale.

Wanasubiru zile nguvu za kuendeshea, ambazo zitamuondoa duniani na kumpeleka utukufuni katika unyakuo. Naamini hilo kwa moyo wangu wote. Ndio Bwana. Hatujui vile atakavyoenda kulitenda hilo, lakini Ataenda kulifanya. Yeye ni zile nguvu za kuendeshea sisitunakuwa tu washirika wa mashine ya mwili wake tukijifanya katika sura yake na tukimuona yeye mwenyewe anaungana na sisi katika kazi zake, katika kipawa chake cha upendo, kadiri anavyotupa hivyo kabla tu ya karamu ya Arusi. Na tunaangalia na kulisubiri hilo.

Kanisa lao kubwa litaunganishwa.

Nguvu za kuendeshea za hili kanisa itakuwa ni kujazwa tena na Roho mtakatifu, ambae tumetenda naye kwa kiwango kidogo wakati kile kifuniko kinakuja chini kuungana na ule mwili. Lakini wakati kichwa na mwili vitakapo ungana pamoja ile nguvu kamili ya Roho mtakatifu itamuinua Bibi Arusi juu, sahihi kabisa kama……….. Hata waliokufa, ambao wamekufa katika kristo kwa miaka mia nyingi iliyopita, watafufuka katika uzuri wa utakatifu wake na kuruka kupitia, mawinguni (1korinto 15:51-54) Nguvu za kuendeshea ni Roho mtakatifu.

Na sasa, nguvu za kuendeshea za utawala huu mkuu ambao inabidi waujenge….. Mashne hii kubwa itatenda kazi moja kupitia muungano wa baraza la dunia baraza la makanisa, ambalo litaweka lazima ya………(ufunuo 13:16-18)

Lakini kumbuka----- unasema, "Hilo litakapotokea…" itakuwa umechelewa sana wakati huo, umeshaingia katika hilo. Kama unataka au hutaki, utakuwa ukotayari hapo. Unaona? Angalia Tayari utakuwa umepata hiyo roho juu yako…….[5]

Maana ya Lutha ilikuwa ni ujumbe wa kuhesabiwa haki ujumbe wa Wesley ilikuwa ni wa udhihirisho wa utakaso; ujumbe wa pentecoste ulikuwa ni kurudishiwa vipawa. Lakini huu ni utambulisho wa kile kifuniko, siku za mwisho, ule mti wa Bibi Arusi. Iko kinyume na vyote hivyo. Na bado ni nuru ile ile kwa waliokomaa. [6].

Mtu mfuaji vyuma anapotengeneza kengele, anayo sauti flani anayotaka aiweke ndani. Anapounda muundo wa kumwagia chuma, anaweka shaba kiasi flani chuma kiasi flani risasi kwa nini? Anajua hasa kiasi cha kuweka ndani ilikutoa mlio sahihi. Na hivyo ndivyo



Yesu alivyofanya kwa Bibi Arusi wake.

Ilibidi aweke kiasi flani Luther, kiasi flani cha Methodist na kiasi flani cha Presbyterian, kiasi flani cha pentekoste ndani. Lakini amepata nini kutokana na hayo? Kuipa sura yake ikiakisiwa. Kwa nini hivyo? Kama tu ule ujumbe wa piramidi. Unaona? Inaenda mpaka inakuja kwenye uchache kwa ajili ya lilejiwe la kifuniko. Huduma ya yesu kristo duniani ilibidi iwe kama ile ile huduma aliokuwa nayo, au vinginevyo hawezi akaja juu yake. Nikama kichwa kilivyo kwa miguu. Miguu sio kichwa, lakini kichwa kinainua miguu au kinaifanya miguu kinaiambia mahali pa kwenda. Unalipata hilo? Ilivyo ya kupendeza. Hiyo ni nuru ya saa hii. [7]

Ndiyo kuwa sehemu ya neno, sehemu ya Neno la leo. Huwezi kuwa na sehemu ya Neno la wakati wa musa. Hiyo sehemu imekwisha kutengenezwa; hiyo ilikuwa ni miguu. Sasa hivi tuko kichwani. Huyu ni kristo. Sio wakati wa Luther mikono nyuma kule; hapana, huu ni wakati wa kichwa. Kristo, Jiwe la kifuniko, linakuja kwenye mwili…. Lile jiwe la kifuniko kinakuja katika mwili kukomboa kile kilicho kombolewa, kuja kuchukuwa walio wake. Yuko hapa pamoja nasi. [8].

Sasa ni maisha gani Luther alikuwa nayo, ilikuwa ni kuhesabiwa haki kwa lmani. Wesley alikuwa na utakaso, uliongezwa kwa hilo. Pentekoste walikuwa na kurudishiwa kwa karama ziliongezwa kwa hilo. Lakini sasa ni kule kukamilisha katika mwili. (unaona?) unaona zile hatua tatu za hilo na kutoka hilo….. wakati ufufuo utakapokuja, maisha yale yalioishi ndani ya hao waluteri, ambao wameshaondoka, uhai ule ulioishi ndani ya wamethodist na wakaondoka, uhai ule uliingia katika wapentekoste, vyote hivyo vitanyakuliwa kutoka ardhini katika mwili wa Bibi Arusi na kuchukuliwa kule mbele za yesu kristo, utukufu kwa Mungu oh inasisimua oh, ni ukweli.

Tumepiga kona. Tunaangalia kuelekea mbinguni, tukitazama kule kuja kwa kifuniko juu ya piramidi kama ambavyo tungesema, kula kuja kwake. Kanisa lazima lifufushwe mapema, na ni lazima tuwe tayari [9]

Na lile jiwe la kifuniko kamwe halikuonekana kamwe hawakuweka kifuniko juu ya piramidi. Sijui kama unalifahamu hilo au la. Lakini kadiri tunavyokua kutoka wakati wa luther, wakati wa wabaptist,

wakati wa Methodist, wakati wa pentecoste. Tuko juu kule kwenye jiwe la kifuniko sasa, tukiwa tunangojea na kwa shauku kubwa kwa lile jiwe la kifuniko likae chini; nyumba imekamilika[10]

Unajua; ile piramidi kamwe haikuwekewa kifuniko, iko hivyo? Kamwe haikuwa na kifuniko kilichowekwa juu yake. Hawakuweza kamwe kukiona. Hawajui kilichotokea kwa hicho. Kwa nini? Kwanini kile kifuniko hakikuwekwa juu yake? Jiwe la juu ya hilo? [10]

Kwa sababu jiwe la kifuniko lilikataliwa; kristo, jiwe la juu, lilikataliwa. [9]

Alikataliwa alipokuja. Alikuwa lile jiwe lililo kataliwa(1petro2:7-8). Hiyo ni sawa. Lakini litawekwa juu. Hiyo ni sahihi. Na halafu yale mawe yanayozunguka kulingana na mzunguko wa jiwe la juu, lazima yatakuwa mawe ambayo yatafanana kwa kikamilifu na hilo jiwe, ambayo yataungana kulingana mahali popote.

Piramidi ni kamilifu huwezi hata kupitisha wembe katikati yao, pale mawe yanapoungana pamoja, uashi ulio mzuri ajabu. Mengine yangekuwa na uzito wa mamia ya tani juu hewani na yanaungana kikamilifu pamoja [10]

Kila jiwe, kadiri linavyofika mwishoni, inabidi likatwe kwa ajilim ya lile jiwe la juu. Sasa, kanisa limekua kutoka lether, Wesley, pentecoste. Inabidi lifikie umbo ambalo kile kifuniko cha juu yesu na kanisa vitakaa pamoja (Halleluyah.) kulifunika juu kanisa lote pamoja kwa ajili ya ufufuko wa kile mwenye mwili ambaye amekufa akiwa analiamini Jina lake. Amen.

Ninaamini tuko hapo leo. Kwamba yesu kristo bado anabakia ni yule jana, leo na hata milele. Unaliamoni hilo?

Sasa na katika Biblia, tunaishi katika siku za mwisho juu ya piramidi, samaki waliokrossiaana wakati wa kensa (saratani) katika zadiaki katika wakati wakuja kwa simba (leo), katika lile jiwe la kifuniko, na katika siku za udhihirisho wa mwana wa Mungu katika Biblia.(warumi8:19-23) unaona? Unaona tuko mahali gani? Tuko hasa wakati wa mwisho. [11].

Mara nyingine tena: kama ile piramidi, jinsi inavyokuja katika uchache wakati wote, kutoka ule mpana mkuu, kutoka luther, Wesley,



pentekoste. Na halafu lile jiwe la kifuniko juu kule lilichongwa; na kila moja ya mawe haya yameshikana pamoja kikamilifu kabisa (na bado hatujajua jinsi walivyofanya hayo); lakini yameshikana kikamilifu katika hiyo piramidi. Na sasa siyo kwamba tunafundisha mafundisho ya piramidi, tuna…… Henoki na wengine walijenga hayo miaka mingi iliyopita na linasimama kama ishara au kielelezo. Kama vile tuu jua lichomavyo na kuzama sawa tu na vile mti unavyodondosha majani yake; yanarudi tena, kama samaki na ng’ombe na kila kitu kinginecho vinaeleleza hilo hiyo piramidi inasimama kama kielelezo.

Nenda katika kile kichumba cha Nabii na uangalie zile ngazi saba. Ni wapi mlinzi alikutana na upinzani kumleta alieingia ili kumpeleka uweponi pa mfalme juu ya zile ngazi? Ilikuwa ni katika ngazi ya saba.

Hapo inaonyesha kuwa lazima tuje tena na Roho yule yule aliekuwa ndani ya yohana; ambaye alimtambulisha masihi. Alikuwa mkuu kuliko manabii wote; kwasababu alimtambulisha huyo(Luka mt.7:24-28)

Na nilazima tufikie mahali tena, kwenye kitu ambacho kitaenda kumtambulisha masihi.

Na nikwajinsi gani watu wanaomwamini yeye watalijua hilo, isipokuwa wadumu kwenye Neno wakati wote ili kujua yeye kile alicho. Daniel alisema wenye hekima watajua, lakini wapumbavu wasio na hekima, hawata elewa. (Wenye hekima) watamjua Mungu wao (Daniel 12:9-10)

Sasa, sasa, jinsi gani alisema litatokea katika siku za mwisho, ilikuwarudisha watu kwenye Neno ili kwamba Bibi Arusi amjue mume wake, amjue mwenzake, Neno lililofunuliwa. Ndio sababu hilo lazima litokee. [12].

Henoki kabla ya maangamizi ya gharika wakati kule kuhesabiwa haki kuna kuja, alileta ishara (kule misri) (lsaya 19:19-20) Na katika hili piramidi kuna ngazi saba kwenda kwenye chumba cha Mfalme. Angalia katika ngazi ya saba (sema uliwahi kujifunza juu ya piramidi). Ni nani anakuja nje kumchukuwa mgeni (ajaye) ili kumtambulisha kwa mfalme, angalia ni kituo cha nani kina simama pale, na utaona siku ambayo unaishi (katika ile piramidi). [13]

Mungu aliandika Biblia tatu. Mojawapo ilikuwa ni ile ya Angani zodiak. Hiyo ndiyo Biblia ya kwanza. Watu walipaswa kuangalia juu

ili kujua kwamba mungu anatokea juu. Fuatia zodiaki; uliwahi kujifunza hiyo? Inakupa hata nyakati zote, hata wakati wa kensa (saratani). Inakupa mwanzoni kule kuzaliwa kwa kristo. Ni kitu gani gani cha kwanza katika zodiaki? Yule Bikira. Ni kitu gani cha mwisho? Yule (lea) simba. Kule kuja kwa kwanza na kule kuja kwa pili kwa kristo vyote hivyo vimeandikwa pale.

Halafu Biblia nyingine iliyoandikwa, ilikuwa katika jiwe, liitwalo piramidi. Mungu aliandika katika piramidi. Kama utajifunza hayo. Angalia historia ya zamani na vita, jinsi walivyojenga kabla ya kuharibiwa na gharika.

Ya tatu iliandikwa katika makaratasi, Biblia. Kwa ajili ya wakati wa werevu, dunia ya wasomi ijayo. Sasa, kama Mungu alivyotenda katika nyakati, tuko kwenye leo yule simba. Tuko kwenye kifuniko cha piramidi. Tuko kwenye kitabu cha ufunuo sura ya mwisho. Sayansi inasema tuko dakika tatu kabla ya usiku wa manane. Oh fikiria mahali tulipo [10]

Mara nyingine tena: katika hii piramidi kulikuwa na ngazi saba na halafu chumba cha mfalme.

Na tuko katika wakati wa saba kabla ya mfalme kuchukuwa kiti chake cha Enzi. Na kumbuka ile piramidi haikuwa na kifuniko juu yake.

Na piramidi ilikuwa iko kwenye hiyo misingi, mpaka juu kule kwenye chumba cha mfalme. Na kabla tu hujafika kwenye ukuta wa saba, kuna mahali padogo pa utambulisho pale, ambapo anakuja mjumbe ili kukuleta kwa mfalme. (yule mjube yahana mbaptisti ambae alimtambulish mfalme--) lakini lile jiwe kuu la pembeni (kifuniko) lilikataliwa. Nao hawajui jiwe lililodharauliwa au vyovyote, viwavyo, hawakujua lilipo kwa sababu ni jiwe lililokataliwa. Lakini hilo ndilo jiwe ambalo linafunika kitu chote, hilo linafanya piramidi katika nyakati kamili saba za kanisa. Ongeza Neema, ongeza hiki, ongeza hiki. Viko vitu saba vya kuongeza, cha mwisho ni kristo. Ongeza hiki katika upendo, ongeza Neema kwenye neema yako, na uongeze kitu kingine na kitu kingine tena, mpaka ifike kwa kristo aliye jiwe la pembeni (kifuniko) “mimi ni mlango” (yohana 10:9)

Waluteri chini ya kuhesabiwa haki kwa imani, ile miguu, iliendelea kama hivyo: Wesley chini ya utakaso. Wapentekoste chini ya mikono



kazi na matendo na kadhalika, ilikuwa kalvinisti…..au iwe watu wa nia au wawe wakisheria. Lakini sasa tunakuja kichwani, kile kifuniko (jiwe) “Neema, Neema” lile jiwe la kuweka juu (kifuniko) lililia (Zakaria 4:6-7).

Lile jiwe la kuweka juu (kifuniko) linalia nini? “Neema Neema” kupita kutoka mautini na kanuni kuingi katika Neno lililo hai la Mungu aliye hai.

Mpango wa Mungu wa pekee kwa wakati wake. Watoto wa Mungu katika wakati wa Neno wakiwa wamehuishwa na Roho kama cheche zilizo washwa na kitu flani kulifanya liwe hai na wakiwa wameketi sasa katika ulimwengu wa kimbinguni katika wakati wa saba (Efeso2:4) tayari wako hai na kila ahadi katika Neno ni yao.

Sasa hilo linafanya nini? Ukiwa sehemu ya chembe ya Mungu, sehemu ya lile Neno, watu wengine ni sehemu ya Neno la Mungu. Wakiwa wameketi pamoja, kudhihirisha mwili wote wa kristo, kwa sababu hakuna chachu miongoni mwenu. (1wakorintho5:6-8). Hakuna chachu miongoni mwenu. Ni lile Neno tu, wameketi katika mahali pa kimbinguni katika mlango ambapo Ameweka jina lake Kristo Yesu [13].

Sasa kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia sana. Kuja kwa hukumu. Anawaita wateule wake pamoja katika umoja na Yeye mwenye, akitumia huduma ile ile aliokuwa nayo mwenyewe. Mnajua kile tulicho onyesha ile sura katika nyakati za kanisa sio muda mrefu uliopita. Juu ya ule mnara mkubwa uliojengwa unaitwa piramidi. Lakini lile jiwe la kifuniko halikuwekwa. Kumbuka jinsi waluteri walivyokuja, halafu Wesley katika uchache, na halafu wakaja tena wapentekoste. Na sasa ni kitu gani anafanya, anaita kutoka hilo. Alifany nini? Aliita wateule watoke kufanya waluteri; A-liwaita wateule kutoka Lutheran kufanya Wesley; Aliwaita wateule watoke humo kufanya Wapentekoste; Sasa anaita wateule wa kipentekoste watoke ili kufanya kile kifuniko kije juu ya hao, huduma ile ile ikishuka pale juu ya hilo, akiita watoto wake watoke katika Madhehebu yote na mtindo wote wa maisha. [14]

Mungu anawachukuwa wateule kutoka katika kanisa la kipentekoste ile mbegu(mchanganyiko), akiitoa itoke nje na kulimalizia Neno. Na inapaswa iwe karibu kiasi kwamba lile Neno lenyewe litaungana na

hili Neno. Hapo sasa kinakuja kile kifuniko, kikilia, “Neema, Neema ya ajabu” lile jiwe la kifuniko, hapa upo kama hivi, pale unaona, jinsi lilivyokuwa pana huku mwanzo? Na linaendelea kuchongwa karibu, karibu karibu (ile huduma), baada ya muda hapa panakuja…… Hapa ni Luther: mwenye haki ataishi kwa imani, amehesabiwa haki. Hapa anakuja Wesley: utakaso: kundi la walio takaswa. Hapa wanakuja wapentekoste: kurudishiwa kwa karama.

Sasa Mungu anachukuwa kutoka pale, akichonga kundi ili kufanya huduma iliyo hasa kama lile Neno pale, kwa sababu inabidi ilingane kabisa na Neno. Huyo hapo Bibi Arusi; anamchukuwa juu.

Vema, sasa hiki ndicho ninacho jaribu kuwaambia ninyi: ile kanuni ya kuzaliwa inaleta kila kimoja kwa jinsi yake (mwanzo1:11). Siku hizi za mwisho, kanisa la kweli Bibi Arusi linakuja kwenye lile jiwe la kifuniko, litakuwa kanisa kuu, mzao ulio tukuka, kadiri wanavyolikaribia lile jiwe kuu la kifuniko watakuwa wanafanana sana na yeye, kiasi kwamba watakuwa katika sura yake ili waweze kuungana Naye; Watakuwa mmoja, watakuwa udhihirisho wa Neno la Mungu aliye hai.

Madhehebu hayawezi kudhihirisha hilo. Watazoa kanuni zao na maungamo yao yakiwa yamechanganywa na Neno na kuleta mbegu ya mchanganyiko. [15]

Halafu kadiri anavyo karibia lile jiwe la kifuniko, anakuwa kama yeye, kwa kupitia neno, yesu atakuja ili Bibi Arusi na Bwana Arusi wawe wameungana milele kama mmoja. [1]

Nukuu za kiingereza.

[1] Laodicean church age- Nyakati saba za kanisa uk.332/363
[2] Kuwekwa wakfu (62-1104E). Aya E-21
[3] Majina ya makufuru (62-1104M). pg 11,15,22,25,
[4] Kimo cha mtu mkamilifu (62-1014M). uk. 47/65
[5] Nimfanyieje mtu aitwae Yesu. Aya 115
[6] Kunamtu anayeweza kuwasha taa (62-1229M) Aya 162/185
[7] Makao ya baadaye Aya 533/373-377
[8] Uongozi (65-1207) Aya 143-144
[9] Wana wa Mungu waliodhihirishwa (60-0518) Aya 47-48
[10] Kule kufanywa wana sehemu ya 4 (60-0522E) Aya 32 20-23
[11] Tunataka kumuona Yesu (60-0708). Aya E-67
[12] Karamu ya baragumu (64-0719M). Aya 110-113



[13] Mahali pekee Mungu alipochagua pa kuabudia 65-1128M Aya 217/262-263
[14] Umoja 62-0211. (kitabu 10 no.2) Aya 183
[15] lile Neno lililo nenwa ndiyo mbegu ya Asili: (62-0318E) uk. 108/119

*jiwe la kiroho la kujengea na 172 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*